#WeweNdoFuture #TimizaWajibu

# HESLB Yako

Jarida la Mtandaoni la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu | Toleo Na. 10

Aprili - Juni 2023

## PROF MKENDA:
## Sera ya elimu itazingatia maslahi ya Taifa



> *"Niwahakikishie hakuna maoni yatakayoachwa bila kufanyiwa kazi! Tutazingatia na tutayabeba kwa ajili ya utekelezaji. Serikali inawashukuru wadau wote kwa kutoa maoni ambayo yamezingatia maslahi ya Taifa"*

Na Mwandishi Wetu
Dodoma

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema kazi ya kukusanya maoni ya kuboresha mitaala na sera ya elimu inaendelea na kwamba maoni yote yatakayopokelewa yatachakatwa ili kupata sera yenye tija kwa Taifa.

Prof. Mkenda aliyasema hayo Mei 14, 2023 Jijini Dodoma wakati wa kufunga Kongamano la wadau wa elimu kujadili sera na mitaala mipya ya elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu lililofanyika kwa siku tatu.

Prof. Mkenda alisema kuwa nia ya Serikali ni kufanya maboresho makubwa kwenye sekta ya elimu na hivyo kamati haitaacha maoni yoyote ambayo yana tija katika kuboresha mfumo wa elimu nchini.

"Niwahakikishie hakuna maoni yatakayoachwa bila kufanyiwa kazi! Tutazingatia na tutayabeba kwa ajili ya utekelezaji. Serikali inawashukuru wadau wote kwa kutoa maoni ambayo yamezingatia maslahi ya Taifa", alisema Prof. Mkenda.

Prof. Mkenda alifafanua zaidi kwamba wapo wadau waliotoa maoni kuwa elimu ya awali iwe ya lazima suala ambalo hata Kamati ya Bunge ilisisitiza na Serikali imelipokea na kuanza kulichakata ili kuangalia uwezekano wa utekelezaji wake.

Hata hivyo, Waziri Mkenda alisema baadhi ya wadau wameshauri elimu ya lazima iwe miaka 11 ikijumuisha elimu ya awali ambayo ni ya lazima. Sera ya elimu ya mwaka 2014 ilikuwa ilipendekeza elimu ya lazima iwe miaka 10 lakini utekelezaji wake ulikuwa miaka 7 na kubainisha kuwa watalifanyia kazi jambo hilo kwa umakini mkubwa.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo Prof. Kitila Mkumbo, alisema wao kama wawakilishi wa wananchi Bungeni watahakikisha wanasimamia maoni ya wadau yafanyiwe kazi kikamilifu ili tija ya kuanzisha zoezi hilo ionze kuoekana baada ya miaka mitano.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (Zanzibar) Bi. Mtumwa Idd Hamad aliwashukuru viongozi wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa miongozo wanayowapa ambayo inarahisisha utendaji wao wa kazi. Bi Mtumwa alisema mabadiliko ya sekta ya elimu yanayofanyika yataleta tija kubwa katika kuhakikisha vijana wanaozalishwa kutoka katika ngazi mbalimbali za elimu wanakuwa na uelewa wa kutosha kuweza kuajirika au kujiajiri wenyewe kutokana na ujuzi wanaoupata.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, alisema michango iliyotolewa na wadau wa elimu itazingatiwa kwenye uchakataji ili kuwa na sera na mitaala bora kwa Taifa.

Sekta ya elimu na mafunzo kwa mujibu wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 na Mpango wa muda mrefu wa Maendeleo ya Taifa 2011/2012 hadi 2024/2025, inatarajiwa kuleta maendeleo ya haraka ya rasilimali watu kwa kutayarisha idadi ya kutosha ya Watanzania walioelimika na kupenda kujielimisha zaidi ili kulifanya Taifa lipate maendeleo na kuwa lenye uchumi wa kati na shindani.

## JAMBO LETU



**Jacqueline Msuya**
*Mhariri*

## Kuelekea kufunguliwa kwa dirisha la uombaji mikopo 2023/2024

Waombaji mikopo wazingatie mwongozo

Tumefunga mwaka wa fedha 2022/2023 na tunaingia mwaka mpya wa 2023/2024 kwa kuwakaribisha pia waombaji wa mikopo ya elimu ya juu ambao watajiunga na vyuo vya ngazi hiyo katika mwaka mpya wa masomo wa 2023/2024 unaotarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Oktoba, 2023.

Kwa kawaida dirisha la maombi ya mikopo kutoka kwa wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na vyuo vya elimu ya juu kwa mwaka wa masomo unaofuata hufunguliwa mwezi Julai kila mwaka ikiwa pia ni mwanzo wa mwaka mpya wa fedha. Maombi haya yanawahusisha wanafunzi waliohitimu kidato cha sita na stashahada ndani ya miaka mitano.

Wakati tunaelekea kufungua dirisha la uombaji mikopo kwa mwaka wa masomo 2023/2024; waombaji mikopo watarajiwa wataanza kupewa taarifa za vigezo, masharti na utaratibu wa kuomba mikopo ili kuwawezesha kuomba kwa usahihi na kupangiwa viwango vya mikopo wanavyostahili kulingana na hali yao ya kijamii na kiuchumi.

Ni muhimu kwa waombaji mikopo watarajiwa kuzingatia maelekezo yaliyomo katika Mwongozo wa Utoaji Mikopo na Ruzuku kwa mwaka wa masomo 2023/2024 uliopo kwa ufasaha katika Lugha mbili za Kiswahili na Kiingereza ukitaja sifa, vigezo, ustahiki wa mwombaji, upangaji wa viwango vya mkopo kulingana na uhitaji na programu atakayopangiwa mhusika kwenda kusoma katika chuo cha elimu ya juu atakachodahiliwa na kinachotambuliwa na Tume ya Vyuo Vikuu nchini (TCU).

Mwongozo wa utoaji mikopo na ruzuku kwa wanafunzi wa elimu ya juu ni taarifa ya wazi inayotangazwa kupitia tovuti ya HESLB www.heslb.go.tz na akaunti zake za mitandao ya kijamii pamoja na vyombo vya habari ili kuwawezesha waombaji, wazazi au walezi wao na wadau wengine muhimu kuusoma na kuuzingatia.

Baadhi ya nyaraka muhimu anazopaswa kuwa nazo mwombaji wa mkopo wa elimu ya juu ni cheti cha kuzaliwa, picha (passport size) ya mwombaji na ya mdhamini wake (mzazi au mlezi), kitambulisho cha mdhamini kimojawapo kati ya vifuatavyo; Kitambulisho cha Taifa, Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, Kadi ya Mpiga Kura, Leseni ya Udereva au Pasi ya kusafiria iliyotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Iwapo mwombaji atazingatia ipasavyo maelekezo ya mwongozo, ni wazi ujazaji wa fomu ya maombi ambao ni kwa njia ya mtandao kupitia https://olas.heslb.go.tz utakuwa rahisi na atatumia muda mfupi sana kukamilisha vipengele vyote vya fomu yake ambavyo vinahitaji taarifa zake binafsi, taarifa za kitaaluma na taarifa za wazazi wake.

Uzoefu wa miaka ya nyuma umeonesha kuwa baadhi ya waombaji wanashindwa kujaza fomu za maombi kwa usahihi na ukamilifu kutokana na kutozingatia maelekezo yaliyomo katika Mwongozo wa Utoaji Mikopo na Ruzuku kwa mwaka husika. Mwaka 2021/2022 kwa mfano, kati ya maombi 95,572, maombi 6,884 hayakukamilika ikiwa ni sawa na 7.2%. Mwaka 2022/2023, kati ya maombi 100,260, maombi 2,997 hayakukamilika ikiwa ni sawa na asilimia 2.9%.

Ni Rai ya HESLB Yako kuwa maombi ya mwaka 2023/2024 yaoneshe tofauti kwa kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi waliojaza fomu zao kwa usahihi na ukamilifu ndani ya muda ambao dirisha la maombi ya mikopo litakuwa wazi.

Kila la heri kwa waombaji wa mikopo na karibuni elimu ya juu.

NDANI...



03 **Balama:** 'Tumsapoti' mama, tujitokeze kurejesha mkopo



06 **Iddah:** Nimelipa wengine wanufaike



08 **Maria:** Wanafunzi vyuo vyote tushirikiane

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Abdul-Razaq Badru

**Katibu**
Omega Ngole

**Wajumbe**
Veneranda F. Malima
Eline Maronga
Jonathan Nkwabi
Jacqueline Msuya

**Designer**
+255 736 190 083

**Mawasiliano**
PSSSF Building,
Makole Road, Plot 4&5,
Block W, Uhindini Area,
P.O. Box 984,
Dodoma, Tanzania

**Simu:** +255 758 067 577/
+255 739 067 577

**Barua Pepe:** adcp@heslb.go.tz
Email: info@heslb.go.tz

**Tovuti:** www.heslb.go.tz

HESLB
BODI YA MIKOPO
INVESTING IN THE FUTURE



# Wanafunzi wengi kunufaika bajeti ya 2023/2024

Nakukaribisha katika toleo la 10 la Jarida hili la Mtandao ili kupata kwa muhtasari yaliyojiri HESLB ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya kila siku na pia matukio muhimu ya kitaifa yaliyofanyika katika sekta ya elimu katika robo ya mwisho ya mwaka 2022/2023.

Kwa kifupi, mwaka 2022/2023 ulikuwa wa mafanikio kwa HESLB na Serikali kwa ujumla katika kuhakikisha utoaji na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu unafanyika kwa ufanisi kwa kutumia mifumo ya TEHAMA na kuzingatia miongozo ya kiutendaji.

Ni matarajio ya HESLB kuwa mwaka 2023/2024 utakuwa wa tija pia katika nyanja za utendaji, uwajibikaji na utoaji huduma kwa wateja ikiwa ni mwendelezo wa ufanisi wa mwaka uliotangulia.

Kipekee nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utashi wake wa kuidhinisha ongezeko la fedha kwa ajili ya kugharimia masomo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Hii inamaanisha wanafunzi wa Tanzania wana uhakika wa kusoma katika ngazi zote za elimu kwa ufadhili wa Serikali.

Shukrani pia kwa usimamizi wa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ikiongozwa na Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda na Bodi ya Wakurugenzi wa HESLB ikiongozwa na Profesa Hamisi Dihenga; chini ya uongozi wao, HESLB imekuwa imara zaidi.

Kwa sasa utoaji wa mikopo ya elimu ya juu unawezeshwa na vyanzo vikuu viwili; ambapo kwa wastani 70% inatoka Serikali Kuu na 30% inatoka HESLB kwenye makusanyo ya mikopo kutoka kwa wanufaika.

Mwaka 2022/2023, Serikali ilitenga TZS 654 bilioni kwa ajili ya bajeti ya kugharimia wanafunzi wa elimu ya juu; kati ya kiasi hicho, TZS 471 bilioni (72%) zilitolewa na Serikali Kuu na TZS 183 bilioni (28%) zilitoka HESLB kwenye makusanyo ya mikopo na kuwezesha kugharimia wanafunzi 202,877.

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST), yaliyowasilishwa na Profesa Adolf Mkenda Mei 16, 2023, Bungeni Dodoma yalielezea utekelezaji wa mpango wa mwaka 2022/2023, vipaumbele, mpango wa mwaka 2023/2024 na kuomba kuidhinishwa kwa jumla ya TZS 1,675,753,327,000/-, kati ya kiasi hicho, fedha za mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ni TZS 738 bilioni.

HESLB ikiwa miongoni mwa taasisi zilizo chini ya WyEST, imepewa kipaumbele kwa kuzingatia majukumu yake ya kuwawezesha wanafunzi wahitaji wa Kitanzania kugharimiwa masomo yao ya elimu ya juu katika fani mbambali. Fedha zilizotengwa bila shaka zitaongeza fursa za mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka wanufaika 202,877 (2022/2023) hadi kufikia wanufaika 210,169 (2023/2024).

Aidha, Waziri Mkenda katika hotuba yake ya bajeti alibainisha kuwa Serikali itaendelea kutoa fursa za Elimu ya Juu kwa wanafunzi wenye ufaulu uliojipambanua kutoka wanafunzi 593 waliofadhiliwa mwaka 2023/2024 hadi wanafunzi 1,200 wanaotarajiwa kunufaika mwaka 2023/2024 kupitia Samia Skolashipu kwenye masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati.

Menejimenti ya HESLB imejipanga kuendelea kusimamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kulingana na ustahiki wa wanafunzi wahitaji wanaolengwa kunufaika kwa kugharimiwa masomo yao kwa mwaka 2023/2024.

> ***"Mwaka 2022/2023, Serikali ilitenga TZS 654 bilioni kwa ajili ya bajeti ya kugharimia wanafunzi wa elimu ya juu; kati ya kiasi hicho, TZS 471 bilioni (72%) zilitolewa na Serikali Kuu na TZS 183 bilioni (28%) zilitoka HESLB kwenye makusanyo ya mikopo na kuwezesha kugharimia wanafunzi 202,877.***

# BALAMA:

## 'Tumsapoti' mama, tujitokeze kurejesha mkopo

*"Naipongeza Serikali, ilifanya jambo jema kuanzisha chombo hiki. Kwa hali na uwezo wa kiuchumi wa familia yangu nisingeweza kusoma elimu ya juu bila mkopo wa elimu ya juu. Sasa mimi ni msomi na najivunia kurejesha ili kuwasaidia wanafunzi wengine wahitaji wanaopambania future zao," anasema Balama.*



Na Mwandishi Wetu
Dodoma

I'm proud kwakweli, ninalipa deni langu kwa moyo mkunjufu. Yaani kwa uchumi wa familia yangu kwa wakati ule nisingeweza kusoma chuo kikuu na kuhitimu.

Robert Fidelis Balama (31), Meneja Takwimu katika Mpango wa Taifa wa Kifua Kikuu na Ukoma - Wizara ya Afya, ni msomi wa Shahada ya Sayansi katika Hisabati na Takwimu kutoka Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mwenge (2013-2016), ambaye anasimulia historia ya elimu na maisha yake.

Hivi karibuni, Balama alielezea namna anavyolipa deni la mkopo wa elimu ya juu kiasi cha TZS 11,483,143.58/- akitoa nasaha kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu kuhusu umuhimu wa kurejesha mikopo hiyo.

"…Tangu naanze kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Isimani nilikuwa nasuasua kutokana na kukosa ada. Baba yangu alifariki dunia mwaka 2007…maisha yakawa magumu zaidi! Hata hivyo, Kutokana na jitihada ya masomo, nilipata ufadhili wa kusomeshwa na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa (2007-2010) na baadae Halmashauri ya Manispaa ya Iringa ikaendelea kunisomesha (2011-2013) kidato cha tano na sita", anasimulia Balama
.

Baada ya kuhitimu shahada ya kwanza mwaka 2016 na kupata ajira katika Hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Iringa kama mtunza takwimu (Data Clerk), ndipo aliamua kuonana na Afisa Rasilimali watu na kumweleza azma ya kulipa deni lake, akasajiliwa kwenye orodha ya watumishi wapya waliosomeshwa na HESLB ili kupata utaratibu wa kurejesha mkopo wake.

Akifafanua zaidi Balama anasema hali ya uzalendo na kujali wahitaji wengine wanaotaka kutimiza ndoto zao za kielimu ndiyo iliyomsukuma kuanza kurejesha mkopo; na kutambua wajibu wake kama mnufaika kwani malengo chanya ya Serikali ni kuhakikisha HESLB inakuwa na Mfuko endelevu unaowezesha wanafunzi wahitaji Watanzania.

"Naipongeza Serikali, ilifanya jambo jema kuanzisha chombo hiki. Kwa hali na uwezo wa kiuchumi wa familia yangu nisingeweza kusoma elimu ya juu bila mkopo wa elimu ya juu. Sasa mimi ni msomi na najivunia kurejesha ili kuwasaidia wanafunzi wengine wahitaji wanaopambania future zao," anasema Balama.

Akirejea uzoefu katika kazi yake ya ukusanyaji taarifa za wagonjwa wa kifua kikuu na ukoma, anasema mafanikio wanayoyapata katika kuwafuatilia wagonjwa ni pamoja na kushuka mpaka ngazi ya jamii ambayo imerahisisha utendaji wa kazi na kuleta tija katika utunzaji wa taarifa na hivyo kufanya ufuatiliaji kuwa rahisi.

Aidha, Balama anatoa wito kwa HESLB kuongeza nguvu na ari ya kuwatafuta wadhamini pamoja na watendaji wa kata waliosaini taarifa za utambuzi wa wanafunzi wakati wa kuomba mkopo, ili watumike kama chachu ya kujua walipo wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu.

"Kipekee ninamshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kufuta adhabu ya 10% ya mikopo pamoja na tozo ya VRF, …hii imeongeza mwamko kwa wanufaika kurejesha mikopo yao bila shinikizo. Nawasihi wanufaika wenzangu "tumsapoti" mama na tuendelee kujitokeza ili HESLB iwe na mfuko endelevu wa kusomesha wanafunzi wengi zaidi," anahitimisha Balama.



*Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru (katikati) akiwakabidhi ngao ya ushindi wawakilishi wa shule za FEZA ambao ni miongoni mwa washindi 10 wa tuzo ya waajiri bora kutoka sekta binafsi waliowasilisha makato ya wafanyakazi wao kwa wakati mwaka huu 2022/2023 wa kwanza kushoto ni Mkurugenzi Msaidizi Urejeshaji Mikopo Phidelis Joseph na wa kwanza kulia ni Meneja wa HESLB Kanda ya Dar es salaam, Anna Sabuni. Hafla fupi ya kukabidhi tuzo hizo ilifanyika Juni 5, 2023 jijini Dar es salaam.*



*Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru (katikati) akiwakabidhi ngao ya ushindi kampuni ya SICPA Tanzania ambao ni miongoni mwa washindi 10 wa tuzo ya waajiri bora kutoka sekta binafsi waliowasilisha makato ya wafanyakazi wao kwa wakati mwaka huu 2022/2023 wa kwanza kushoto ni Mkurugenzi Msaidizi Urejeshaji Mikopo Phidelis Joseph na wa kwanza kulia ni Meneja wa HESLB Kanda ya Dar es salaam, Anna Sabuni. Hafla fupi ya kukabidhi tuzo hizo ilifanyika Juni 5, 2023 jijini Dar es salaam.*




*Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Abdul-Razaq Badru (mwenye tai nyekundu) akiwa katika picha ya pamoja na washindi 10 wa ngao kutoka Taasisi binafsi za Dar es salaam baada ya kuwasilisha kwa wakati makato ya wafanyakazi wao waliokopeshwa na HESLB. Hafla fupi ya kukabidhi tuzo hizo ilifanyika Juni 5, 2023 jijini Dar es salaam.*



*Mheshimiwa Dr. Samia Suluhu Hassan akimpa mkono wa pongezi mfanyakazi hodari wa HESLB mwaka 2023, Erick Mathias katika sherehe za Mei Mosi zilizofanyika Mkoani morogoro tarehe Mei 1, 2023*



*Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) Dkt. Franklin Jasson Rwezimula (wa pili kulia) akiteta jambo na Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Abdul Razaq-Badru (wa kwanza kulia) na Mkurugenzi wa Urejeshaji na Urejeshwaji Mikopo George Mziray (wa kwanza kushoto) alipotembelea ofisi ya HESLB, Dar es salaam Aprili 12, 2023. Wengine kwenye picha ni maafisa wa WyEST na HESLB.*




*Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Prof. Jamal Adam Katundu (kulia) akisalimiana na Kaimu Meneja wa Kanda ya Arusha, Sunday Charles Katika maonesho ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) yaliyofanyika Mei 16-22, 2023 katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.*

# SINGA:

## HESLB inaongeza ufanisi kidigitali

*"Kabla ya mwaka 2019, fedha zilikuwa zikitumwa vyuoni na wanafunzi kusaini kwenye orodha za malipo kwa njia ya karatasi na baadae fedha kuwekwa kwenye akaunti za wanafunzi…" anaelezea Singa.*

Na Mwandishi Wetu
Dodoma

Mkurugenzi Msaidizi wa TEHAMA – HESLB Bahati Singa, amesema takribani huduma zote za HESLB zinapatikana kwenye mifumo na kwamba HESLB imejipanga vyema kuwahudumia wateja wake kupitia mifumo yake iliyoboreshwa zaidi.

Singa ameelezea changamoto mbalimbali zilizokuwepo huko nyuma zilizosababisha HESLB kuboresha mifumo yake ili kuongeza ufanisi kwenye utendaji kazi na kurahisisha utoaji huduma kwa wateja wake.

"Kabla ya mwaka 2019, fedha zilikuwa zikitumwa vyuoni na wanafunzi kusaini kwenye orodha za malipo kwa njia ya karatasi na baadae fedha kuwekwa kwenye akaunti za wanafunzi…" anaelezea Singa.

Sambamba na changamoto hiyo ya malipo, Singa amesema HESLB imepitia vipindi mbalimbali hadi kufikia uboreshaji wa mifumo iliyopo sasa, ambapo awali waombaji wa mikopo walikuwa wakiwasilisha maombi yao kwa njia ya fomu za karatasi, wanafunzi kutopata mrejesho kwa haraka na wakati mwingine vyuo kuchelewa kurejesha HESLB fedha za wanafunzi wa mwaka wa kwanza ambao hushindwa kufika chuoni au kwa wale ambao wamesitisha masomo.

Akifafanua zaidi kuhusu mifumo mahsusi iliyoboreshwa, Singa amesema mifumo inayohusiana na uombaji mikopo, ulipaji wa mikopo na urejeshaji wa mikopo hiyo imeboreshwa na kuongeza tija katika kutoa huduma kwa wateja.

"Maboresho makubwa yamefanyika kupitia mfumo wa OLAMS (Online Loan Application and Management System), ambapo kwa sasa kupitia akaunti ya SIPA ya mwanafunzi mnufaika wa mkopo anaweza kupata taarifa zake katika hatua mbalimbali….", anasema Singa.

Kuhusu mfumo wa malipo wa kidigitali (DiDiS), Singa ameelezea jinsi mfumo huo ulivyoweza kupunguza gharama kwa taasisi, na umerahisisha wanafunzi kupata malipo yao kwa wakati kwa kutumia simu janja ama tovuti kwa wale ambao hawana simu janja.

"Kwa sasa mfumo huu wa DiDiS (Digital Disbursement Solution) umeunganishwa na mfumo wa malipo ya Serikali na benki na kwa mara ya kwanza kwa mwaka ujao wa fedha (2023/2024), malipo ya ada yatalipwa moja kwa moja kwenye akaunti za vyuo kwa njia ya mfumo…, anasisitiza Singa"

Kwa upande mwingine, Singa amesema DiDiS pia imerahisisha mchakato wa kurejesha fedha HESLB kwa wanafunzi ambao hawatasaini malipo yao kwa kutumia alama za vidole ndani ya muda (siku 30) uliopangwa.

Akizungumzia mfumo wa urejeshaji mikopo, Singa amesema EPO (Employers' Portal) imeboreshwa ili kumwezesha mwajiri kupata taarifa ya hatua mbalimbali za madeni ya wanufaika wa mkopo wa elimu waliopo kwenye taasisi yake.

Singa ameongeza kuwa, bado maboresho ya mifumo yanaendelea na mingine ipo katika hatua za mwisho, ikiwemo kumwewezesha mnufaika wa mkopo anayerejesha mkopo kupata barua kwa njia ya mfumo, kuthibitisha kukamilisha kulipa mkopo wake wote.

Singa amesisitiza kuhusu utayari wa HESLB katika kuhakikisha huduma bora inapatikana kupitia kwenye mifumo na kusema kuwa, HESLB imejipanga vyema kutoa huduma zake kupitia mifumo na inaendelea kuiboresha zaidi ili kurahisisha upatikanaji wa huduma, kupunguza muda wa kupata huduma na kuondoa malalamiko ya wateja.




# IDDAH:

## Nimelipa wengine wanufaike

Na Mwandishi Wetu
Dodoma

Mwalimu Idda Phillemony Mwakibinga wa Shule ya Msingi Area 5 iliyopo Nanenane mkoani Morogoro amejitokeza na kulipa mkopo wake wote wa elimu ya juu baada ya kuona umuhimu wa kurejesha kuwawezesha watanzania wengine wenye uhitaji nao wapate fursa ya kusoma elimu ya juu.

Mwalimu Idda anasimulia safari yake ya kupata taaluma hii ya Ualimu ilipoanzia, kwa kupata cheti cha Ualimu baada ya kuhitimu mafunzo katika Chuo cha Ualimu cha Kilutheri Uyole mwaka 2007 na kuajiriwa katika Shule ya Msingi Kiwira Coal Mine (KCM). Mwalimu Idda aliamua kujiendeleza zaidi mwaka 2012 hadi 2014, ambapo alipata Stashahada ya Ualimu katika chuo cha Teofilo Kisanji (TEKU) na mwaka 2015 alijiunga na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), ambapo mwaka 2018 alihitimu na kutunukiwa Shahada ya Elimu.

"Wakati nasoma Shahada yangu, nilikopeshwa na serikali kiasi cha TZS 9,400,000/- kupitia Bodi hii ya Mikopo, na nashukuru iliniwezesha kusoma katika mazingira mazuri huku nikipata mahitaji yangu ya kujikimu…", anaelezea Mwalimu Idda.

Kuhusu sababu iliyomsukuma hadi kufanya maamuzi ya kulipa mkopo wake wote, Mwalimu Idda anasema amekuwa akiona watu wakilalamika kwa kukosa mikopo ya elimu ya juu ili kutimiza ndoto zao. Hali hiyo imekuwa ikimsononesha na hivyo kuamua kujipanga na kulipa deni lake lote akiamini litakuwa msaada kwa mnufaika mwingine.

"Nimekuwa nikiona watu wa karibu na wakati mwingine kusikia kupitia vyombo vya habari, vijana wakilalamika wamekosa mikopo ya elimu ya juu ili kutimiza ndoto zao, nikaona ni vyema nijipange nilipe deni langu lote ili na mwingine asaidike…", anasema Idda

Kwa upande mwingine, Mwalimu Idda ameishukuru Serikali kwa kuendelea kuwasomesha vyuo vikuu watanzania wahitaji kwa kuwakopesha kupitia HESLB, na anawasisitiza wanufaika wa mikopo kuwa wazalendo kwa kurejesha mikopo yao kwa wakati mara tu wanapopata kipato.

Aidha, Mwalimu Idda ameishauri HESLB iendelee kutoa elimu kwa wanufaika hasa kwenye eneo la utaratibu wa kurejesha mikopo akielezea kwa upande wake kuwa hakupata taarifa mapema ya nini cha kufanya alipotaka kurejesha hadi alipoamua kufunga safari na kufika ofisi za HESLB.

"Naishauri HESLB itoe elimu ya kutosha kuhusu utaratibu wa kurejesha mikopo hii, maana naamini kuna wengine kama mimi wana nia ya kurejesha mikopo yao lakini hawajui waanzie wapi…", anasisitiza Mwalimu Idda.

# Utekelezaji wa majukumu ya HESLB kupitia mradi wa HEET

> ***"Kupitia mradi wa HEET, HESLB imeanza kuboresha mifumo yake ya utoaji na urejeshaji mikopo kwa kuboresha uhusiano na wadau wa kimkakati, kuwajengaa uwezo watumishi wa HESLB na kuimarisha taratibu za kutambua Wanafunzi wahitaji na urejeshaji wa mikopo ili kuwa na mfuko endelevu…".***

HESLB ni moja kati ya taasisi 22 zilizo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia zinazotekeleza Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) wa miaka mitano unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Mratibu wa mradi wa HEET- HESLB, Gertrude Alphonce amesema kuwa HESLB kupitia mradi wa HEET tayari imeanza kutekeleza majukumu yake kwa kuhuisha utaratibu mzima wa utoaji na urejeshaji mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu ili kubaini maboresho yanayoweza kufanyika ili kuleta mabadiliko chanya katika sekta elimu ya juu.

"Kupitia mradi wa HEET, HESLB imeanza kuboresha mifumo yake ya utoaji na urejeshaji mikopo kwa kuboresha uhusiano na wadau wa kimkakati, kuwajengea uwezo watumishi wa HESLB na kuimarisha taratibu za kutambua Wanafunzi wahitaji na urejeshaji wa mikopo ili kuwa na mfuko endelevu…".

Gertrude amesisitiza kuhusu maboresho makubwa ya kimfumo yanayoendelea kupitia mradi wa HEET na kufafanua kuwa, "Kupitia mradi huu wa HEET, HESLB inaendelea na maboresho ya mifumo ya uombaji mikopo (OLAMS), upangaji mikopo (ILMS), ulipaji mikopo kwa wanafunzi vyuoni (DiDiS), pamoja na urejeshaji mikopo (ERP), ambayo tunaamini itasaidia katika kuongeza ufanisi kwenye utoaji na urejeshaji wa mikopo."

Gertrude ameongeza kuwa, HESLB kwa kushirikiana na wadau kutoka taasisi za elimu ya juu na za kifedha, ilifanya tathmini tatu zinazolenga kuleta mabadiliko kwenye ugharimiaji wa elimu ya juu kupitia kongamano lililojumuisha pia Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia.

Licha ya tathmini hizo, Kongamano pia lilitumika kupokea maoni yenye lengo la kuziboresha na kuwasilisha Wizarani ili kupata maelekezo yenye kuleta mageuzi katika ugharimiaji wa elimu ya juu.

Tathmini ya kwanza ilikuwa juu ya athari za elimu bila ada kwa shule za sekondari kwenye utoaji wa mikopo ya elimu ya juu na ililenga kubainisha jinsi (HESLB) inavyopaswa kujiandaa kwa ongezeko kubwa la wanafunzi wahitaji wanaotokana na elimu ya msingi na sekondari bila ada.

Tathmini ya pili ilihusiana na vipaumbele vya masomo ambavyo HESLB huzingatia katika kukopesha mikopo ya elimu ya juu na hali ya soko la ajira lilivyo kwa sasa.

Tathmini ya tatu ilihusiana na vyanzo vingine vya fedha ili kuwezesha wanufaika wengi zaidi wahitaji wanaojiunga na elimu ya juu waweze kukopeshwa.

Sambamba na tathmini hizo, HESLB pia katika mwaka huu 2022/2023 imetembelea taasisi tatu (3) zinazotoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu zilizopo kwenye nchi zingine za Afrika (Msumbiji, Ghana na Kenya) kwa lengo la kujifunza kwa kuangalia sera zao kwenye utoaji na urejeshaji mikopo, namna mifumo yao ya utendaji inavyofanya kazi na huduma kwa wateja zinavyotolewa ili kuleta mabadiliko chanya kwenye mikopo ya elimu ya juu nchini Tanzania.

Gertrude anaamini kuwa mradi wa HEET wa miaka mitano, utakuwa na mchango mkubwa katika safari ya mapinduzi katika ufadhili wa elimu ya juu na kuchochea mageuzi ya kiuchumi Tanzania.

# MARIA:
## Wanafunzi vyuo vyote tushirikiane



*"Mchakato ulianza kwa wagombea nane (8) ambao wote tulikuwa wanawake, tukatangaza nia na baaadae mmoja hakurudisha fomu, watatu waliamua kujitoa na mwisho tulibaki wagombea wanne (4) ambao ndio tulipigiwa kura….", anaelezea Maria.*

Na Mwandishi Wetu
Dodoma

Rais wa Shirikisho la Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu Tanzania (TAHLISO), Maria John Thomas amewakumbusha wanafunzi wa vyuo vyote nchini kuendelea kushirikiana katika kulinda na kutetea maslahi ya wanafunzi ili kuleta amani na utulivu vyuoni.

Maria ambaye ni mwanafunzi wa mwaka wa tatu wa Shahada ya Sanaa na Elimu katika Chuo Kikuu cha Jordan kilichopo Morogoro, alichaguliwa kuwa rais wa TAHLISO Aprili 1, 2023 na kuanza kazi rasmi Aprili 14, 2023 baada ya kuapishwa kutumikia nafasi hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Maria ni rais wa kwanza mwanamke wa TAHLISO na amesema, jambo angependa kuliona ni vyuo vyote kuungana na kushirikiana kwa kutatua changamoto kwa pamoja ili kuwa na mazingira rafiki kwa wanafunzi kuweza kusoma na kutimiza ndoto zao.

Akizungumzia safari yake kuanzia mchakato wa uchaguzi hadi kufikia kuchaguliwa kushika nafasi ya urais wa TAHLISO, Maria amesema alikutana na ushindani wa kawaida na kwa mara ya kwanza wagombea wote waliojitokeza kugombea nafasi hiyo ya urais wa TAHLISO, walikuwa ni wanawake.

"Mchakato ulianza kwa wagombea nane (8) ambao wote tulikuwa wanawake, tukatangaza nia na baaadae mmoja hakurudisha fomu, watatu waliamua kujitoa na mwisho tulibaki wagombea wanne (4) ambao ndio tulipigiwa kura….", anaelezea Maria.

Katika kutekeleza dhamira yake ya kuwa na ushirikiano zaidi na vyuo vyote, Maria ameeleza kuwa TAHLISO imejipanga kuwa na ziara ya kutembelea vyuo vyote nchini kwa lengo la kupokea changamoto zilizopo kwenye vyuo hivyo ili kuzitafutia suluhisho kuwezesha uwepo wa mazingira mazuri ya wanafunzi kusoma.

Kuhusu Mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu, Maria ameishukuru Serikali kwa kuendelea kutenga bajeti ili kuwawezesha wanafunzi vyuoni kutimiza ndoto zao, na kwamba yupo tayari kufanya kazi kwa ukaribu na HESLB ili kutatua changamoto mbalimbali za mikopo ya elimu ya juu zinazotokea vyuoni.

Katika hatua nyingine, Maria ameiomba HESLB kupitia miongozo na vigezo vinavyotumika katika kutoa mikopo ili kuwafikia wahitaji wengi zaidi, ikiwemo kufikiria uwezekano wa kuanza kutoa mikopo kwa wanafunzi ambao wapo kwenye vyuo vya kati.

Maria amewakumbusha pia wanafunzi wa vyuo vikuu kujitambua na kuendelea kutimiza wajibu wao wa kusoma na kufaulu ili kufikia malengo yao. "Wanafunzi vyuoni tujitambue, tutambue kwanini tupo vyuoni, tuishi utanzania wetu kwa kuzingatia maadili yetu…." anasisitiza Maria.

**HESLB**
Loans Board
INVESTING IN THE FUTURE

# Strategic Plan 2022/2023 - 2026/2027
# WE VALUE

## VISION
To become a reliable and sustainable Tanzanian financier for tertiary education students.

## MISSION
To sustainably issue loans and grants to eligible Tanzanians pursuing tertiary education & prudently manage loans collection.

## STRATEGIC THEMES
- Optimal lending and loan collection
- Business re-engineering and automation
- Strategic partnerships

## CORE VALUES

### ACCOUNTABILITY
We take the initiative to own our responsibilities by pursuing excellence, honouring our commitments and upholding integrity.

### CUSTOMER – CENTRIC
We are committed to prioritize and timely serve, listen and respond to customers' needs.

### TEAMWORK
We embrace networking and support one another in pursuit of excellence in serving customers.

### PROFESSIONALISM
We are qualified, skilled and passionate in delivering our services in accordance with highest standards of ethics.

### INNOVATION
We constantly develop solutions to address new lessons to meet the evolving needs of our customers.

### EQUITY
We treat our customers with fairness and respect to promote diversity and inclusion.

HESLB Tanzania | HESLB_Tanzania | 0739 665 533

HEET | WORLD BANK GROUP

## OUR PROJECT:
### Higher Education for Economic Transformation

**Description:**
- HEET is a USD. 4 million, five-year (2021/22 – 2025/26) project funded by the World Bank to promote reforms and improved operational capacity and delivery at HESLB.

  The project is steered by the Ministry of Education, Science and Technology
- **Project Development Objective:**
  To strengthen the learning environments and labor market orientation of programs in priority disciplines and the management of the higher education system
- **Component 2:**
  Strengthening the management of the higher education system

**Project Focus Areas**
- Business process re-engineering
- Performance and operational improvements on loans management
- Strengthening coordination and linkages with stakeholders
- Capacity building of staff
- Public-private partnerships
- Developing new policies to support equity, quality and sustainability.


OUR CONTACT

**DODOMA**
PSSSF Building, Makole Road, Plot No. 4&5, Block W. Uhindini Area,
P.O. Box 984, Dodoma, Tanzania
+255 758 067 577
+255 739 067 57
dodoma@heslb.go.tz

**DAR ES SALAAM**
HESLB House, 1 Kilimo Street, Tazara Area, Mandela Road,
P.O Box 76068, 15471 Dar es salaam, Tanzania
+255 739 665 533, info@heslb.go.tz

**ZANZIBAR**
Michenzani Mall Building, Michenzani Area, Side A,
5th Floor, Hall 501
P.O. Box 900
Zanzibar, Tanzania
+255 779 321414
zanzibar@heslb.go.tz

**MBEYA**
CAG Building, Mbalizi Road
P.O. Box 319
Mbeya, Tanzania
0738 131310
0738 131311
mbeya@heslb.go.tz

**ARUSHA**
NSSF Mafao House, 1st Floor,
P.O Box 2712,
Arusha, Tanzania
+255 27 2520128
+255 624 100011
+255 0739 102016
arusha@heslb.go.tz

**MTWARA**
NHC Raha Leo Complex
2nd floor Plot no. 217 Block H.
Near Regional Commissioner's Office
P.O.Box 969,
Mtwara, Tanzania
Cell: 0736 026 668
mtwara@heslb.go.tz

**MWANZA**
PSSSF Plaza Building, 2nd Floor Front Wing, Kenyatta Road,
P.O. Box 3051,
Mwanza, Tanzania
+255 28 2506008
+255 759 819350
+255 738 153661
mwanza@heslb.go.tz

**CUSTOMER CENTRE**
PSSSF Twin Towers,
Ground Floor,
Plot 120/121, Mission Street,
P.O. Box 76068,
Dar es salaam.